



## TAARIFA KWA UMMA

### TANGAZO LA KUANZA RASMI KWA UTOAJI WA HUDUMA ZA AFYA KWA WANACHAMA WA ZHSF IFIKAPO TAREHE 09/10/2023

IMETOLEWA NA WAZIRI WA AFYA

**MHESHIMIWA NASSOR AHMED MAZRUI**

#### **Ndugu wananchi;**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya inaendelea na jitihada za kuhakikisha inawapatia wananchi wote wa Zanzibar huduma bora za afya. Kama tunavyofahamu kuwa katika kufanikisha juhudi hizo, Serikali ya Awamu ya Nane chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, imeanzisha Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar kupitia Sheria Na. 1 ya mwaka 2023.

Hivyo, Serikali kupitia Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF) inapenda kuwaarifu wanachama wote katika Sekta ya Umma kwamba, ifikapo tarehe 09/10/2023 huduma za afya kupitia Mfuko wa ZHSF zitaanza kutolewa rasmi katika vituo vya Serikali na vya binafsi ambavyo vimesajiliwa na Mfuko. Orodha ya vituo hivyo inapatikana katika tovuti ya Mfuko [www.zhsfsmz.go.tz](http://www.zhsfsmz.go.tz)